



## REPUBLIC OF KENYA

### COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

#### THIRD ASSEMBLY- THIRD SESSION

##### THE HANSARD

Wednesday, 17<sup>th</sup> April 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

*[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]*

##### PRAYER

##### MOTION

#### ADOPTION OF THE REPORT ON THE FORMALIZATION OF THE MZAMBARAUNI, MAZERAS MUGUMO WA PATSA AND KIBOKONI SQUATTER FORMALIZATION SCHEMES

**Hon. Ray:** Thank you, Mr. Speaker, I wish to move the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Lands, Energy, Housing, Physical Planning and Urban Development Committee on the formalization of the Mzambarauni, Mazeras Mugumo wa Patsa and Kibokoni Squatter formalization schemes laid on the table of this House on Tuesday, 16<sup>th</sup> April 2024.

Before I call hon. Jambo to second this Motion, may I inform this House that the proposed Mazeras Mugumo wa Patsa, Kibokoni and Mzambarauni settlement schemes were Tabled on 11<sup>th</sup> March 2024 pursuant to Standing Order 120. The documents were committed to the sectoral Committee on Lands, Energy, Housing, Physical Planning and Urban Development. Also pursuant to Article 196 Section One of the Constitution of Kenya, 2010 and Standing Order 120 (3); the Committee invited members of the Public to submit memoranda and the Committee

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

received one memorandum. Further, more members of the public were invited for a public participation exercise of these various schemes on Thursday, 28<sup>th</sup> March 2024. This exercise took place at Shimo la Tewa; that is at Mzambarauni Hall and Deliverance Church from 10.00 a.m. to 2.00 p.m. on Tuesday. The public participation took place at Rabai Kisurutini Ward, Jesus Fire Ministry and Rabai Social Hall that was at 10.00 a.m. and 2.00 p.m. respectively.

On Wednesday, it took place at Sabaki Ward which is at Sokomoko Balozi at 10.00 a.m. and Kibokoni Baptist at 2.00 p.m. After public participation, we went for a Report compilation that is from the 4<sup>th</sup> to the 6<sup>th</sup> of April 2024 and we got some findings and recommendations. One of them is some people were not present during the picking of boundaries and the Committee had not reached out to them. Another finding was that some of the residents there gave their plots for public utility, but the issue was on the compensation. They had not been compensated and there we talked with the committee and the County Government of Kilifi to make some arrangements for the payment before the end of the exercise.

Mr. Speaker, at the Committee we made some recommendations that the adoption of Mzambarauni, Mazeras Mgumo wa Patsa and Kibokoni N27 informal settlement scheme to be passed...

*(Hon. (Ms.) Maneno stood on a Point of Information)*

**Hon. Ray:** Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): So, hon. Ray, would you like to be informed by hon. (Ms.) Mary Maneno.

**Hon. Ray:** No.

**Hon. (Ms.) Maneno:** Mr. Speaker, Sir, I want to correct something which is supposed to be on record. We have 'Mugumo wa Patsa' not 'Mugumo wa Pasta' kindly because these things are on record.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Thank you hon. (Ms) Mary Maneno.

**Hon. Ray:** That was a typing error, thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Hon. Ray who is seconding you?

**Hon. Ray:** Hon. Jambo.

**Hon. Jambo:** Thank you, Mr. Speaker, I rise to second.

*(Question proposed)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): I am not able to see any request from the Members. Kindly allow me to now put the Question.

*(Question put and agreed to)*

ADOPTION THE REPORT OF THE PICPAC COMMITTEE ON THE CONSIDERATION OF THE REPORTS  
OF THE AUDITOR GENERAL OF THE FINANCIAL YEAR ENDED 30<sup>TH</sup> JUNE 2021 ON THE KILIFI  
COUNTY EXECUTIVE FINANCIAL STATEMENTS

**Hon. Thaura:** Thank you Mr. Speaker for this opportunity, I beg to Move a Motion that this House adopt the Report for PICPAC...

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Hon. Munyoki stood on a Point of Order)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): You are rising on which Point of Order?

**Hon. Munyoki:** The Member is not properly dressed. Kindly guide him.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Sergeant-at-Arms, check the Member to see if he is properly dressed?

**Hon. Thaura:** I can correct that very quickly before...

*(The Sergeant-at-Arms escorted Hon. Thaura out of the Chamber)*

*(Hon. Thaura entered the Chamber)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Thank you, hon. Munyoki, for that observation. Hon. Member, you are a senior in this House that should not happen.

**Hon. Thaura:** Mr. Speaker, I want to apologize before these honourable House for that slight mistake. I had started making my contributions that I stand to move a Motion:

THAT, This House adopts the Report of the PIC/PAC Committee on the consideration of the Reports of the Auditor General on the financial year ended 30<sup>th</sup> June 2021 on the Kilifi County Executive Financial statements.

Before, I call upon the seconder who is hon. Mohamed, let me give my submissions. This Committee did its job in looking into these Reports. The Committee closely examined the Reports of the Auditor General on the financial statements of the Kilifi County Executive for the financial year 2021 ending 30<sup>th</sup> June as I cited.

In this exercise, the Committee was guided by the principles as well as the rules, procedures and customs of the County Assembly derived from the Constitution of Kenya 2010, the Act of Parliament, the Kilifi County Assembly Standing Orders, conventions and practices and ruling the directives of the Chairperson. The minutes of the Committee are annexed at the end of this Report and can be obtained in the HANSARD.

The Committee made sure we understood what the Department has been doing and we have in this Report given the observations and recommendations of this very able Committee. In the observations, the Committee noted that there is poor performance by some of the officers, particularly with respect to failure to respond to management letters from the Auditor General. It is ideal for the Officers to make sure they respond in good time and with valid Reports to the Auditor General's Office, but this never happens.

The other one is poor response to the audit queries; the officers seem to have no clue of some of the queries that the Committee and the Auditor General tried to seek from them. Then we have another issue which is the late submission of some of the Reports. The other thing is numerous excuses for not doing all these things that are already cited. Close to 60% of the audit queries in these Reports have been resolved by way of belated action by the County Officers upon being invited by the Committee. So, had it not been for the Committee requesting them to appear before, probably they would not have given the documentation to the Auditor General's Office.

This would probably not have been the audit queries for the Accounting Officers, had they effectively and promptly responded to the Auditor General's letters and provided the necessary supporting documents. In most cases, the Accounting Officers act on queries just when

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

it is about to appear before the Committee. So as a Committee, we noted there is laxity in the Departments, we are worried about why the Officers cannot provide the documents and even before the Committee, most of the documentation was not appropriate, sometimes, the dates did not marry.

As a committee, we cited that there was the failure to provide documentation at the right time, provide invoices and payment vouchers and receipts. We made recommendations, as a committee, that any officers who are not doing their job well be named in public and scrutinized. As a committee, we did a noble job, and I would wish that this able House adopts these Reports and every recommendation that was put across to be taken seriously. Thank you, I welcome my Deputy Chairperson to second.

**Hon. Mohamed:** Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity to stand and second the Report but before I second, I would also wish to submit that the PIC/PAC Committee through the wisdom of the Chairperson as he has submitted, scrutinized this Report and we found out that there are numerous mistakes which had resulted from the Auditor's opinion of this Report. Among the observations that we found in this Report which is not supposed to be a practice is the late submission of imprest of some officers authorized to them.

In this Report, we have imprest which was supposed to be submitted by officers who are not even within or working with the County Government of Kilifi by now. These imprests have not been surrendered up to now. It was or is an issue which the Committee picked up and we have recommended very severely that going forward, the Accounting Officers who will have authorized imprest given to Officers within the County Government of Kilifi and who have not submitted their imprest should not be given any other imprests or the Officers concerned will be surcharged because we do not want any public money for Kilifi to get lost. There is a need for the officers in charge, which I believe even this House witnessed when His Excellency the Governor of Kilifi appeared in the Senate. It was well addressed and as the Chairperson has said the Implementation Committee which will be handling this will have to make sure that these imprests have been submitted because if not, they will appear in the next Audit Report. When it comes to the next Audit Report, it will not be business as usual for the PIC/PAC Committee. Since the Chairperson has submitted much of the Report, especially the observations and recommendations, then I stand to second the Motion. Thank you.

*(Question proposed)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): I do not see any request, maybe the system is not working well. If anyone wants to speak you can kindly raise your hand, so hon. Shehe you may proceed.

**Hon. Shehe:** Thank you Mr. Speaker, Sir. I stand to support the Motion. The PIC/PAC Committee did their best. As they commented, I think there is a big problem with some of our officers either they do not know what they are doing, or it is very deliberate. We were having a very hot debate with the County Attorney, and we were trying to trace them because there was a very big problem. Any Bill that goes to the other side is supposed to be threshold discussed within them and sent to the Governor for assent. That is not happening. Some of the Bills that were discussed in this honourable House have been pending and we do not know the fate of those Bills to date. And that is exactly what our able colleagues here were commenting on the same. There is a need to call the relevant Officers instead of just mentioning them. They should

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

come and speak to this House to show cause whether they know what they are doing or their assumptions are wanting because we are not here for a football game as just spectators. Once something has been done here, it is decided, and we expect results from relevant avenues, and we are left without any interpretations of what has been discussed.

I throw the ball back to maybe the Legal Department to follow up with the Officers who are relaxing. We do not have answers and even in the other meetings that we had, the Officers were hands-off because the big boss is untouchable, or he didn't want anything to be followed up. We said nobody is above the law and we are here, and some people have overrun the Departments in such a manner that what they do is what they need and is not followed. I stand to support, and they did a very good job, but we have a lot to do. Thank you.

**The Deputy Speaker (Hon.Kombo):** Hon. (Ms.) Mary Maneno.

**Hon. (Ms.) Maneno:** Thank you Mr. Speaker, Sir. I rise to support the Motion on the adoption of the Report of the County Public Investment and Accounts Committee on the consideration of the Reports of the Auditor General of the Financial Year Statements of the Kilifi County Executive for the financial year ending 30<sup>th</sup> June 2021.

Hon. Speaker, the Chairperson has submitted a comprehensive Report, I therefore urge the Accounting Officers to take the auditing process very seriously because auditing has stages and to avoid coming with Reports to the Committee which were supposed to be taken to the Auditor General. Mr. Speaker, Sir, I remain supportive on the adoption of this Report. Thank you.

**Hon. Brown:** Thank you, Mr. Speaker. Our colleagues in PIC/PAC did a very wonderful job. It has reached a time that this honourable House should stand and make sure we narrate our mandate. As you have heard, the Report is very vital. We need to make sure that we have a framework of making sure these officers whom we vetted and gave them jobs should be in order and competent to make sure that they do what is required. We likely need to see that the work being done is for the benefit of *mwananchi* from this County and not somebody that does what they think. Equally, it is our mandate as the oversight team to make sure that we are making some framework of what we always pass in this Assembly. Let us not have the culture of passing things and we do not make follow ups. The Implementation and PIC/PAC teams must make follow ups and we should not be used as puppets in this honourable House. Thank you, I stand to support this Motion.

**Hon. (Ms.) Grace:** Asante, Bw. Spika, kwa hii nafasi. Nasimama kuunga mkono Ripoti ya PIC/PAC. Nimeskiza Mwenyekiti sana vile alivyoongea na yangu ni machache. Nasubiri kuona wakitenda kazi. Hao maofisaa ambao hawafanyi kazi nasubiri kuona wakichukuliwa hatua kwa hivyo Bw. Mwenyekiti na Kamati yako niko hapa nikisubiri kuona hiyo kazi ikitendeka. Asante.

**Hon. Zia:** Asante, Bw. Spika. Kongole kwa Kamati husika ya PIC/PAC kwa kuja na hii Ripoti. Ni kati ya wale ambao wanaunga mkono hii Ripoti hasa nitaongelea vile hii Ripoti iko. Nimetamaushwa sana kwa jinsi vile pesa za umma huwa zinachukuliwa na maofisaa wetu wa kaunti. Ni aibu na sasa imefikia wakati Bunge hili liweze kusimama na kuhakikisha kwamba inatekeleza majukumu yao. Kuna mambo mengi ambayo yanafanyikia ndani ya hii Kilifi haswa upande wa *Executive*, kuna utepetevu uko na hakujakua na ule msukumo wa kisawasawa kama Bunge na inatupasa sisi sote iwe ni changamoto ambayo tukilalia kidogo mambo mengine yanaharibika ndani ya hii kaunti. Ni jukumu letu na kila mmoja achukue jukumu lake kikamilifu ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa kikazi unafanyika. Kuna mambo mengi ambayo

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

yamefanyika sana, tukiangalia mbali na hii Ripoti, hata zile Ripoti ambazo ziliweza kutangulia ya kwamba kuna maofisaa wengine walilalia kazi mahali. Magari yetu yamepotea, gari zengine zimefichwa mahali.

Ukiangalia katika Ripoti hii nayo unapata kwamba kuna wengine wamekua na pesa muda huo wote lakini hakuna hatua ambayo imechukuliwa. Nikaachiwa mimi hapa hakuna kubembelezana kwa sababu mwisho wa siku yule ambaye anaumia ni yule mwananchi. Pesa inafujwa lakini hakuna chochote ambacho kinafanyika. Hii serikali yetu ya Kaunti ya Kilifi bado nina shaka nayo sana. Ikiwa kama tutaachilia na tuendeleo vile ambavyo iko, zaidi ya mamilioni ya pesa yataendelea kupotea na wananchi watakua wanaumia kule.

Hii Ripoti ni lazima hatua zichukuliwe haswa Kamati ya Utekelezaji nikiwa mimi ni mmoja wao na Mwambire na Thaura ni mmoja wao. Kwa hivyo, tukitoka hapa ni lazima Mwenyekiti Meshimiwa Changawa asimame pia na sisi tuungane mkono na yeye ili kuhakikisha kwamba hii Ripoti inatekelezwa kwa kikamilifu ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kama ilivyopendekezwa na Ripoti ambayo imeletwa hapa. Asante.

**Hon. (Ms.) Mariam:** Asante, Bw. Spikia, kwa fursa hii. Mimi pia nasimama kuunga mkono hii Ripoti na pia nipongeze Kamati kwa kazi nzuri ambayo mumeifanya na unajua hii ni Kamati ambayo tunaitegemea sana ndani ya hili Bunge. Ukiangalia kwa maswala ya ukaguzi wa fedha zinatumiwa vibaya kwa hivyo ni Kamati moja muhimu sana na Mwenyekiti na timu yako nawapongeza kwa hii Ripoti. Nataka kuzungumzia hii Ripoti haswa kulingana na hii pesa ambayo inachukuliwa kwa Kizungu inaitwa *imperest*. Kwa ufahamu wangu, nafahamu kuwa hii ni pesa ambayo ina muda wa kuregesha na ni masaa 48. Sasa tukiskia hapa kuna watu mpaka wametoka katika hii Kaunti kwa miaka na bado wako na hii pesa basi nafikiri kama Kaunti hatuko vizuri katika hali ya kulinda ile rasilimali ya wananchi.

Na sisi kama watu tuliopewa jukumu la kuona kuwa mali ama fedha za mwananchi zikija ndani ya hii Kaunti zimetumiwa kikamilifu kulingana na sheria, nafikiri kama Bunge tuko na kazi na tukiangalia *recommendations* za Kamati, ziko sawa. Kama wenzangu walivyotangulia kusema sasa ni ile Kamati ambayo itafwatilia ambayo ni *Implementation* na uzuri wale ambao wako kwa PIC/PAC nimeona pia ni wana Kamati kwa hii Kamati. Mimi pia nikiwa Mwenyekiti mdogo wa hio Kamati nafikiri tuko na jukumu kubwa sana ndugu zangu kuhakikisha rasilimali ya Kilifi imemfaa mwana Kilifi na sio wana Kilifi wachache kwa sababu wale walioenda na pesa ni wachache lakini wengi ni wale ambao wanahitaji huduma.

Bwana Spika, kitu chengine ambacho nimekiangalia katika hii Ripoti, kuna kitu ambacho pia nataka kuzungumzia katika hii Ripoti; maswala ya muda. Kila kitu ndani ya serikali kina muda. Kitu ambacho kina shangaza ni kuwa maafisaa wetu wanashindwa kupeana stakabadhi kwa wakati unaostahili. Na ni swala ambalo wao wanajua. Ukifika wakati huu, tunatajikana tuwe stakabadhi hizi tumezikabidhi mahali fulani. Lakini utapata mpaka *Auditor General* akija chini bado hawa watu hawajapeana stakabadhi. Stakabadhi za *tender* ambao ni kitu kinaanza huko mwanzo lakini mpaka *Auditor General* akifika hizi hazijapeanwa hapo kidogo unakuwa na tashiwishi.

Zile stakabadhi ambazo wana peleka baadaye ni nani atahakikisha kuwa hizi ni stakabadhi za uhakika? Na kama ni za uhakika, kwa nini hazikuwa kuanzia mwanzo? Bw. Spika na waheshimiwa wenzangu, tuko na kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa rasilimali ya Kilifi tunailinda kama vile Katiba ilivyo tupatia hilo jukumu. Asanteni sana.

**Hon. Hinzano:** Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia fursa hii kuweza kusimama katika Bunge lako hili tukufu kuweza kuchangia hii Ripoti ambayo imeletwa hapa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Bungeni na waheshimiwa. Kwanza, ninaunga mkono kwa ukamilifu kabisa na pia vile vile niweze kutoa mapendekezo yangu juu ya hawa maafisa ambao wako katika ofisi lakini wameweza kujisahau. Ninaweza kusema ni kujisahau na mara ingine naweza sema ni makusudi tu.

Hii ni kwa sababu jukumu ambalo waliwekewa kwa ofisi wanalijua vizuri na kama ni kutayarisha stakabadhi mapema, wana uwezo huo. Lakini shida ni kwamba kuna shida kubwa katika hii serikali kwa sababu mimi nikiwa katika mrengo wa Kenya Kwanza naamini kabisa serikali ya Rais William Samoi Ruto inaleta pesa mapema na hii pesa inafaa kuja kwa Kaunti ya Kilifi. Kila Kaunti inapatiwa pesa yake, sasa nikiona watu wamejipanga mahali kwa ofisi kuweza kuchukua hiyo pesa na kuitumia vibaya ni huzuni kubwa sana. Mara ingine huwa nina jiuliza sisi tumekosea wapi? Na ninaona lawama nyingi sijui mambo ya serikali kuu, lakini tujiulize hii serikali yetu ya Kaunti ya Kilifi hizi shilingi milioni zaidi ya kumi na tatu (13) ambazo zina kuja zina tumika vipi ndio iwe tu tunaweza kulalamikia tena serikali ya juu.

Serikali Kuu haina makosa yoyote kupeleka pesa kwa Serikali ya Kaunti na kila kaunti inapata pesa yake. Lakini kuna maafisa, mheshimiwa Spika, ambao wamejipanga wao na familia zao na kuwaacha wananchi wakiteseka. Imekuwa ni desturi na wakati tulipokuja hapa kuwahoji, mimi hata nilikuwa sitaki kutumia hizi nakala ambazo zilikuwa zimechapishwa kwa sababu hapa pia kuna watu wanazipata mapema kupatiwa ili wakija hapa wawe wanaelewa kila swali ambalo linaulizwa hapa, mimi huwa situmii hiyo.

Maswali yangu huwa ni rahisi tu, sasa hivi unasema wewe uko sawa je ukiingia kwa ofisi utakuwa sawa kama hivyo ama unasema kwa sababu unataka hii kazi? Na wanasema huwa wanasema wako sawa lakini baada ya muda unakuta kwamba lile swali, halija jibika ni kwamba wanafanya tu kijifanya lakini wana mipango mingine mibaya sana. Ni huzuni kubwa sana, watu wana teseka, watu wanahangaika lakini maafisa ambao wako katika ofisi na kuna wakati mmoja nilimwambia Gavana, tulipitisha ndio sisi hatuna makosa kupitisha kwa sababu kwanza tuliangalia stakabadhi zao na tukaona ni sawa, hatujafanya makosa yeyote.

Ikiwa kuna afisaa ambaye analeta ulegevu wa kazi, pia ni jukumu la Gavana kutuletea hilo jina hapa Bungeni. Hajaambiwa yeye akae hapo milele wala haja gongolewa misumari hapo. Ikiwa kuna makosa ambayo yanafanyika, ni jukumu la mheshimiwa Gavana huyu afisaa aletwe kabla haja haribu mambo kwa sababu mambo yakiharibika hata angaliwa yule afisaa ambaye yuko katika ofisi, anayeangaliwa ni mkuu wa kauti ambaye ni Gavana. Kwa hivyo, ninaunga mkono Ripoti hii na ile Kamati ambayo ni ya utekelezaji pia msiwe na uoga uoga na vitisho ambavyo mnatishwa tishwa ovyo ovyo na kuanza ati kuogopa ogopa. Mkiogopa, wanaoumia ni wananchi, kwa hivyo bora utoke; kama uko moto uwe moto na kama ni baridi uwe baridi, hakuna mambo ya kuwa vugu vuguili tuhakikishe kwamba kila kitu kina enda sawa.

Waheshimiwa, mimi ninataka niwaambie hivi; uongozi unatoka kwa Mwenyezi Mungu na ukisimama kwa ukweli na haki, Mwenyezi Mungu ana kuongoza na mambo ya kutishwa sijui kuna mwaka wa 2027 huo mwaka hayo ni mambo mengine kabisa. Sasa hivi tumepatiwa majukumu mwaka wa 2022 mpaka 2027 kwa hivyo ni tufanye kazi hapa kwa yule mwananchi aliyetuchagua hapa. Sio mambo ya kunitisha hapa sijui mwaka wa 2027 sitaingia. Atakayeingia pia ni mwanadamu bora awe ni mwana Kilifi lakini mimi nimefanya wajibu wangu hayo mambo ya mwaka wa 2027 mimi sitaki kujua. Kile ninataka kujua kwanini pesa ya Kilifi inaletwa na haiendi kwa yale mambo ambayo yanafanyika ndani ya Kilifi? Mimi ninaunga mkono Ripoti hii na hiyo Kamati ya Utekelezaji iweze kufuatilia na kuhakikisha kwamba kila kitu kina kuwa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sawa. Haya si mambo tena ya kuchezeana, hata unaweza sema mpaka 2027 utaingia na Mwenyezi Mungu achukue roho yako, utaenda fanya nini wapi?

*(Laughter)*

Tufanye kazi sasa hivi mambo yanayo kuja na mambo ya huko mbele yaachie Mwenyezi Mungu. Yeye Mwenyezi Mungu ukisimama na ukweli atakutolea njia hata kama kuna pingamizi gani hakuna mtu anaweza zuia maamuzi ya mwenyezi Mungu. Asante sana, mheshimiwa Spika.

*(Applause)*

**Hon. Ngirani:** Thank you, Mr. Speaker, I stand in support of this Report done well by our able Committee PIC/PAC led by my good neighbour hon. Thaura Mweni aka *bulldozer*. From the Report, it is evident that the problems that are being implicated by the Auditor General are generally caused by the Executive officers themselves. If you talk of pending bills, pending bills are something that is being caused by the Executive accounting officers. This is because you will see a situation whereby a project done three weeks ago is being paid for and a project done years ago is pending. They always compile or rather pile these pending bills themselves because there is no proper system of payments with our Treasury.

Personally, there is a project that was done some years back in Ganze. It was completed but up to date that project has not been paid for yet there is a project that was done just two or three months ago, and it has been paid. I think, Mr. Speaker, it is high time this House came up with a Motion that we pay these contractors and suppliers on a first come first served basis.

The delay in Quarterly Reports is there. This House received Quarterly Reports for various Departments. Various Committees receive these quarterly reports, but these reports normally come with a very big delay. You can witness one case whereby we are in the fourth quarter maybe and a department has not submitted even the first or second quarter reports. The Committee writes to the Executive requesting these quarterly reports. Some quarterly reports come copy pasted. You see a quarter report of the first quarter report the same as the third quarter report, so they are not serious about coming up with these quarterly reports.

Mr. Speaker, I think it is high time the Executive is willing to support the Chief Executive who is the CEO (Chief Executive Officer) of this County, the Governor in implementing his manifesto. It is high time these officers pulled up their socks in working for the implementation of the manifesto of the Governor.

Mr. Speaker, there are so many incomplete projects as per these reports. This report was done two years ago but the same problem is recurring. Even up to date, we have incomplete projects some were from 2020 and 2021 even to date, they are stalled. I think all these problems which come out in the Auditor General's Report, these problems can be cured through the seriousness of our Executive Officers or the people responsible for implementing these things; these are the big issues that are causing problems in this County with the Auditor General in Nairobi. It is high time if an officer is not competent, let him or her step aside, let us get competent officers who are going to work and will not put us in hot soup with the Auditor General. Thank you, Mr. Speaker, Sir.

**The Deputy Speaker (Hon.Kombo):** Hon. Tete.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*



**Hon.Tete:** Asante, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii nichangie mawili matatu katika hii Hoja. Kwanza, ninaunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya PIC/PAC kwa uzuri na wema ambao wamefanya kuangazia Bunge hii kuyajua yale ambayo hatungeweza kuyajua isipokuwa kupitia kwao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kusema ya kwamba kwanza hii serikali mahali imefika uzuri na wema ubaya na ubaya wake, naamanisha hii serikali kuu kwanza ikiwa ni njema, kuna nyengine ilikuwa njema hii iliyoko saa hii inaiga. Ikiwa ni ubaya, ubaya uliko ulichangia serikali zengine tukazitoa tukaona hii kwamba inaweza kutusaidia. Inaaminisha kwamba sisi hapa mashinani serikali ilete pesa kwa wakati wa sawa, matumizi yetu ndio muhimu, ichelewe ikifika matumizi yetu ndo muhimu.

Hatutaponda serikali kuu kwa ubaya ulioko, tutaangalia zaidi hapa kwetu kwa sababu ichelewe, ifike mapema tuna maswali ya kujiuliza inapoingia kwa gatuzi letu la Kilifi, hii fedha inafanya kazi namna gani? Moja, hii Bunge isiwe ni kama ni Bunge ya kutengezea watu ajira na wananchi wanateseka. Ninakumbuka tukiwa hapa, kama Mheshimiwa Hinzano alivyosema, ya kwamba tulikuja hapa tukajaribu kuwadadisi waliokuwa wamepeana maombi yao ya kazi hususan nyadhifa hizi za *Chief Officers* na Mawaziri. Kwa kiwiliwili ukiwaangalia walikuwa ni watu unaweza fikiria kuwa wanaweza na hawataweza kutubwaga katika lugha nyepesi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, tusihukumu vitabu kwa kurasa za kwanza. Mara nyingi tutajikuta yaliyoko ndani ni mabaya kuliko yaliyoandikwa kwanza na ndivyo walivyo maafisa wetu katika Kaunti ya Kilifi hii. Viongozi ambao wamepea nyadhifa ni sawa sawa na rais muovu anayetumia jeshi kuhakikisha yuko salama. Nikilinganisha hii hali na taifa jirani hapa Uganda, watu wanalalamika sana kwamba hafai, hafai, lakini panapo tokezea mtu kuzungumza atapitia mateso mengi sana kiasi cha kukosa kujua alikuwa inastahili kuongea kwa niaba ya wananchi ama ni vile ilivyo baki na ikiwa nikubaki vile, mwananchi atakuja lini mahali kama hapa kujizungumzia?

Sisi tuliotumwa, na ninashukuru Kamati ya PIC/PAC ya kwamba wewe hukutumwa na mheshimiwa yoyote hapa yakuenda fanya ile kazi. Ni sheria imewapatia uwezo. Ripoti hii isibebe mtu ya kwamba fulani amefanya hivi, kama ni ubaya uko na hiyo Kamati na imefanya kazi yake. Sisi lazima tujue na tuwakilishe wana jamii wetu ili wajue ni kipi chaendelea chema na kibaya. Nina ni nani anasimama kwa niaba ya jamii? Viongozi ama maofisaa wetu ambao tumewaweka kwa ofisi, sisi pia tunaangaliwa na miaka mitano ikiisha, Mheshimiwa Spika, kama alivyo zungumza Mheshimiwa Hinzano, hakuna atakaye baki na atakaye baki ana kipindi chake cha kuenda pia. Hivyo ndivyo ilivyo kwa hii Bunge walioanzisha hawako na sisi pia twapita, kwa hivyo, hatutaogopa kuzungumza yale ambayo yanajiri yasiyo kuwa na misingi ya kujenga jamii. Tuyanyamazie kwa sababu ya kuwa naogopa kesho yangu, mimi naichukua kesho yangu naiweka kwa Mwenyezi Mungu nikijua yeye ndiye alinipangia kesho yangu.

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuuliza uzito na uzani wa hii Bunge wakati maofisaa kama hawa wanaendelea kudhalilisha Serikali yetu ya Kaunti kwa utendaji kazi wao, dawa yao iko hapa ama inapatikana wapi?

*(Loud consultations)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Juzi tulikuwa na *legal team*, matamshi yaliyosemwa pale yalinitatiza. Idara zinasemekana kwamba wengine hawafanyi kazi na kama nikuletwa hapa Bungeni, hili Bunge limezoeleka, hakuna chochote kitafanyika. Nilistaajabu sana kwamba tunazoeleka kiasi gani? Yaliyotuleta hapa tunayafahamu ama ni nani ana tu *compromise* kiasi cha kwamba tuende sawa sawa na vile tunavyobebwa kule. Ni ombi langu, Mheshimiwa Spika, kuwa kila mmoja abebe msalaba wake. Wakati tukipiga kampeni ya kusema ya kwamba tunafaa si kwamba tulikua tunafaa kwa sababu, samahani nitaingiza lugha nyingine ya, “*Mgiriama kutsomwa ni nguo, si kuifwa mlume bure*”. Kwa hivyo, lugha hii naizungumza hapa mwenye kusikia asikie na kama kuna tafsiri itazungumzwa baadaye. Tusijenge misingi ya kupendeza kwa mavazi na kuonekana kwamba sisi ni bora kumbe ubora hatuko nao.

**The Deputy Speaker** (Hon.Kombo): There is an intervention from hon. (Ms.) Grace.

**Hon. (Ms.) Grace:** Bw. Spika, naomba mheshimiwa aliye kwa sakafu kuna lugha ambayo ameiongea ambayo hairuhusiwi hapa na si kila mtu anasikia na sijui amesema nini. Ninaomba aweze kufafanua ili na sisi wengine tuweze kujua amesema nini, tusije tukawa tumeitikia kumbe anatuza.

*(Laughter)*

**Hon. Tete:** Asante, mimi imani yangu inaniambia kwamba unayafahamu japo si lugha ya hapa. Lakini nataka kukufahamisha hii ya kwamba si kila mwanaume ambaye anapendeza kwa mavazi ana asilia ya kwamba yeye ni kidume. Kwa hivyo, nyanjani kule wakati tukiuzia sera tukizungumzia ubabe ya kwamba naenda na yaweza isionekane kwamba ilikua wakati ule tumejivisha tuonekane kuyaweza kumbe si kweli na ndio hii Bunge isidhalilishwe; tusifanane na mavazi, acha tuachilie ukakamavu tuliokuwa tunauzungumzia nje wakati wa kampeni.

Na hii Bunge isidharauliwe na mfanyikazi yoyote aliyekuja hapa kuja kuomba kazi akaeleweka na hatimaye ule mtazamo tuliomuona nao sio alio nao kule. Na mimi pia nasikitika sijui tutatumia lugha gani, mheshimiwa Spika, ya kuwajua watenda kazi wakati wameleta makaratasi yao na kule nje hatuwezi kuwajua ni wakati gani walifanya mema ndio tukawapatia kazi. Kwa hivyo, mimi machungu yangu ni kwamba hii Bunge inadhalilisha waheshimiwa. Tunabebwa kwamba hakuna lolote ambalo tunaweza kufanya kwa hizo Idara.

Na mimi kama nitafanana na wengine watakao kuwa nyuma yangu siku moja waendeleo kufanya hivyo lakini tukipatana kama ishirini na watano (25) tukisema waje watakuja kusema kitu. Na hii kama iko kwenye mitandao iangaziwe. Hatutakubali hii serikali yetu na wananchi wetu waendeleo kuteseka huku wachache wakitajirika kujijenga na watu wanaendelea kuumia.

Mheshimiwa Spika, hiyo Ripoti ya NARIGP (*National Agricultural and Rural Inclusive Growth Project*) bado sijaridhika nayo. Sijaridhika nayo na hapa hapa kwa sports hapa, twendeni vizuri bado tunaona kuna shida. Na kwa ajili ya matumizi ya pesa ya umma mheshimiwa ugeni umeniisha. Wakati tukiwa tunaomba mikopo kama *House Leadership, House Business* tulijaribu pia kufuatiliza mambo ya kusema tunataka hata ripoti ama *statement of account* ya mikopo ya hapa. Mwaka umeisha na zaidi na hiyo ni pesa ya umma ambayo inatusaidia sisi kufanya yale ambayo tunaweza kuyafanya. Ni wapi hapo ambapo tunaweza kuitisha kwa haraka hiyo ripoti ikapatikana na tukajua ni kipi ambacho kinaendelea?

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Tunataka hiyo ripoti pia hapa tui pate na matumizi jinsi mambo yalivyoenda. Tusipewe mikopo tukarudisha kilichoingia hatujui kimezaa nini ni ngapi kimebaki hatuna miaka ijayo tunarudishwa hapa hapa wengine wakija ni wageni hawajui pa kuanzia hawajui pa kumalizia, mambo yanasonga tu hivyo hivyo. Ule ugeni umetuisha na tunataka kila kitu ambacho kinastahili kufanywa kwa ajili ya faidi ya mwana Kilifi kimefanyika kisawasawa.

Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi, hawa auditors ambao huwa wanatembelea hizi ofisi zetu ikiwa sisi kila siku tuna lalamika kwamba kuna uovu huwa wanaponea vipi wakati sisi kila siku tukija hapa tunasema kuna uovu lakini *Audit Report* hiyo mwaka unaenda kuko sawa; wa pili wa tatu mpaka Bunge msimu unaisha hakuna aliyechukuliwa hatua. Huyu alipatikana na hatia na sisi kila kukicha tunasikia nje ya kwamba kuna ufasidi. Basi nasema kwamba kilicho chini kisikie na kilicho juu kisikie. Ninachotarajia mimi ni kuona kwamba kuna hatua fulani zimechukuliwa kutetea pesa ya umma na ikiwa mbebaji yupo, basi abwage mzigo atetee nafsi yake. Asante.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Tete, kwa changizo zako za hekima na uzito mwingi.

*(Question put and agreed to)*

#### ADJOURNMENT

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Hon. Members, the House stands adjourned. Thank you.

The House rose at 3:40 p.m.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*